# SHINDANO LA FANIKISHA BIASHARA

**Limeandaliwa na Tanzania Cigarette Company Limited**
**Tanzania Entrepreneurship and Competetiveness Centre**

## KIFURUSHI CHA TAARIFA KWA WASHIRIKI

Kifurushi hiki cha Taarifa kwa Waombaji wa kushiriki katika Shindano laFanikisha Biashara kina mambo yafuatayo:

1. Sifa za kushiriki Fanikisha Biashara TEAM Challenge
2. Sheria za Fanikisha Biashara TEAM Challenge
3. Sheria zingine za Fanikisha Biashara TEAM Challenge
4. Hatua/Mchakato wa Fanikisha Biashara TEAM Challenge
5. Mchakato wa kupata washindi
6. Zawadi za Fanikisha Biashara
7. Taarifa za mawasiliano
8. Fomu ya Maombi Fanikisha Biashara TEAM Challenge (itumwe TECC)
9. Maelekezo kuhusu Wazo la Biashara
10. Hati ya kukubali Masharti ya kushiriki Fanikisha Biashara TEAM Challenge (Itumwe TECC)

## 1. UTANGULIZI

Unakaribishwa kushiriki katika Shindano la Fanikisha Biashara TEAM Challenge mwaka 2022, inayoandaliwa na Tanzania Cigaratte Company Limited (TCC) ikishirikiana na Tanzania Entrepreneurship and Competetiveness Centre (TECC).

Fanikisha Biashara TEAM Challenge ni fursa kwa biashara zinazopenda kupanuka, kwa Team za vijana wa kike na kiume waliojiri kibisahra na wasio na ajira ambao hawapo shuleni, vijana waliomaliza vyuo hivi karibuni, kuwasilisha Mpango wa KUKUZA Biashara ambao utafanyiwa tathmini na jopo la wataalam, wafanyabiashara na washauri waliochaguliwa kutokana na weledi wao.

Lengo la Fanikisha Biashara TEAM Challenge ni kuwapa vijana washiriki ujuzi na maarifa ya kukuza biashara, na motisha muhimu ili kukuza biashara endelevu katika mazingira yao na ya ushindani ambayo yanawakabili katika changamoto za kukuza biashara zao. Mitaji ya fedha na elimu ya kuendeleza biashara itatolewa kwa washindi watatu ili kusaidia kupanua biashara zao. Fanikisha Biashara TEAM Challenge itawakutanisha na taasisi za mikopo na vijana ambao watakuwa tayari wameiva na na wameonyesha juhudi kubwa wakati wote wa shindano hili.

Fanikisha Biashara TEAM challenge itapokea maombi kupitia njia ya mtandao au njia zingine za kisasa ikiwa ni jitihada ya makusudi kuwasukuma washiriki watumie fursa za kimtandao katika kupanua na kukuza biashara zao. Fomu za maombi za Fanikisha Biashara TEAM Challenge zitapatikana kwa urahisi kutoka mtandao wa TECC na kwa njia ya kawaida kutoka kwa TCCIA, TWCC na Afisa Vijana wa Wilaya za Kondoa na Iramba.

TECC

TCC

Washiriki wakiisha kuchukua fomu, watazijaza na kuziwasilisha kwa mtandao info@tecc.co.tz. Kiambatanisho hiki kinatoa taarifa kuhusu taratibu, sheria, sifa za kushiriki na mchakato wa kuendesha mashindano.

## 2. SIFA ZA KUSHIRIKI/SHERIA ZA FANIKISHA BIASHARA TEAM CHALLENGE

**Wote wanaopenda kuomba kushiriki katika FANIKISHA BIASHARA TEAM CHALLENGE watatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-**

**Sifa za Kushiriki;**

a) Wawe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaoishi au kufanya shughuli zao nchini
b) Wawe na umri miaka 18-35.
c) Vijana wawe watatu au zaidi ambao ama tayari wanafanya biashara pamoja au wanakusudia kuunganisha biashara pamoja.
d) Kuwa tayari kuweka saini Hati ya kukubali masharti ya kushiriki (angalia ukurasa wa mwisho) na iwapo watachaguliwa wataweka saini Hati ya Makubaliano.
e) Washiriki ni lazima wao binafsi washiriki katika warsha zote za mafunzo ya Fanikisha Biashara TEAM Challenge.
f) Majaji, Wakufunzi, Wataalamu na wafanyakazi wa TCC, TECC, TCCIA na Serikali Kuu au Serikali ya Mtaa HAWARUHUSIWI kushiriki katika Shindano.
g)

Taratibu za msingi/sheria za kuwasilisha na kutathimini Mpango ya Biashara:

a) Mpango wote wa Biashara ni lazima uwe unahusu biashara zinazolenga kutengeneza faida. Biashara zisizolenga kutengeneza faida haziruhusiwi kushiriki.
b) Mpango wa biashara uwe una uwezo wa kuwa endelevu na uwe wa biashara halali.
c) Mpango wa Biashara upendekeze kupanua biashara iliyopo nchini Tanzania.
d) Mpango wa Biashara unaopendekezwa uwe katika sekta inayokua, mfano, kilimo na usindikaji, viwanda, utalii au huduma. Jedwali lifuatalo linaonyesha vigezo vya kutambua ukuaji vitakavyotumika katika tathmini ya mwanzo.

| **AINA YA BIASHARA** | **MIFANO YA MAWAZO YA BIASHARA YENYE KUKUA** | **MIFANO YA MAWAZO YA BIASHARA ISIYOKUA** |
|---|---|---|
| Uzalishaji Viwandani | Kutengeneza matofali, Bidhaa za ngozi, utengenezaji chaki, vinyago, kutengeneza majiko ya nishati jadidifu, nguo, kuseketa, kuweka rangi nguo, samani, sehemu za mashine za makanika, kutengeneza sabuni za miche na unga, kazi za kutengeneza vyuma n.k. | Kufanya biashara ya bidhaa zilizokwishatengenezwa. Mfano kuuza duka, kuuza maji, kuuza soda, kuuza nguo kutoka nje ya nchi |

| | | |
|---|---|---|
| Nishati | Uzalishaji na usambazishaji nishati hususan mbadala na zinazo linda mazingira. | Kukuza tekinologia ambayo haizingatii mazingira. |
| Madini | Uchimbaji mdogo mdogo wa madini bila kuharibu mazingira na kuchonga mawe | Kununua na kuuza mawe au vito vya thamani bila kuyakata na kuyasafisha. |
| Biashara ya kilimo na kusindika vyakula | Kusindika asali, Mafuta na Juisi za matunda, kusindika vyakula, kusindika bidhaa za wanyama, mvinyo, kusindika karanga, n.k., kwa kuuza kibiashara | Kilimo kwa ajili ya chakula au ufugaji wa wanyama au biashara ya bidhaa za kilimo zizizosindikwa |
| Utalii | Utalii wa asili unaolenga soko la ndani na nje, utayarishaji/usindikaji wa bidhaa zenye kulenga soko la utalii, nk. | Biashara ya udalali kwenye huduma za utalii na nyumba za wageni |
| Huduma | Elimu, Afya, huduma za mifugo, Huduma Bunifu za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano nk. | Ushauri, utaalamu wa masoko na huduma zingine zisizoongeza thamani. |

e) Kila Mshiriki atatakiwa kuwasilisha Mpango wa Biashara moja tu katika Shindano hili. Washiriki watakaowasilisha zaidi ya wazo moja wataondolewa katika shindano.

f) Mpango wa Biashara uwasilishwe MARA MOJA tu,

g) Mpango wa Biashara ni lazima uwe wazo binafsi la washiriki na siyo la kuletewa na mamluki.

h) Mpango wa Biashara NI LAZIMA uandikwe katika Microsoft Word kwa Kiswahili katika Times New Roman Font Size 12. Maombi yatakayoandikwa kwa mkono HAYATAFIKIRIWA. (Angalia maelekezo ya mpango wa Biashara).

i) Washiriki lazima waambatishe picha zao za karibuni kwenye fomu ya maombi.

**3. Sheria zingine za Fanikisha Biashara TEAM Challenge**

***Maombi yawasilishwe kwa wakati kwa kuzingatia muda wa maombi uliowekwa (Kati ya tarehe 19 Novemba 2022 hadi 02 Desemba 2022. Hakuna maombi yatapokelewa baada ya Ijumaa tarehe 02 Desemba 2022. Maombi yatakayochelewa hayatapokelewa. Maombi yakiishawasilishwa hayataweza kubadilishwa***.

4. Malipo kwa ajili ya maombi: Hakuna malipo yoyote yatakayolipwa wakati wa kujaza Fomu ya Maombi. Hata hivyo, mtu akichaguliwa na kualikwa katika mafunzo ya siku moja hadi mwisho

a) Mara baada ya mpango wa biashara kuwasilishwa itakuwa ndiyo mwisho. Hakuna maombi mengine yatakayopokelewa tena kutoka kwa Mjasiriamali huyo.

b) Majaji, Wakufunzi, Waelekezi na Waandaaji watachukua tahadhari kubwa katika kutunza siri.

c) Washiriki watatakiwa kuwepo wao binafsi pamija na timu yake ya watu wawili katika vituo kuhudhuria mafunzo na kuwasilisha mipango yao.
d) Kila Mshiriki ni lazima akubali masharti ya shindano na kuweka saini Hati ya kukubali kushiriki.
e) Washiriki ni lazima wakubali ya kwamba taarifa zao za usajili na binafsi zitaweza kutumika kwa ajili ya uchambuzi wa kumbukumbu na kuitangaza Programu.
f) Maingizo yote katika Shindano yatabaki ni kuwa mali ya wamiliki wenyewe kisheria.
g) Mshiriki ni lazima awe na/au awe tayari kufungua Akaunti ya Benki ili kuweza kupokea ruzuku.
h) Mitaji ya shindano haiwezi kuhamishwa, kupitishwa kupitia mtu mwingine au kuongezewa muda
i) Mitaji itatolewa kulingana na Sheria za Tanzania ikiwa ni pamoja na Sheria za Kodi ambazo zinaweza kuwahusu baadhi ya washiriki.
j) Mitaji hii ni mtaji wa biashara. Watakaopata ni lazima waitumie kwenye biashara zao ndani ya miezi mitatu tangu walipopokea mitaji. Aidha kama mitaji haitumiki ndani ya miezi mitatu, taarifa zipelekwe kwa TECC mara moja.
k) Matumizi ya mitaji ni lazima yawekewe kumbukumbu za Ankara na stakabadhi za fedha ambazo zitatumwa ofisi za TECC kwa ukaguzi na ufuatiliaji.
l) Waombaji watatakiwa kufuata maelekezo haya na taarifa zingine zitakazotolewa na TECCau taarifa watakazopewa wakati wa kuhudhuria mafunzo na ambayo yatatolewa katika mtandao wa TECC.
m) **UTUNZAJI WA SIRI:** Mpango wako wa Biashara utatunzwa kwa siri kubwa. Waandaaji wote, wafadhili, majaji na waelekezaji ni watu wenye ueledi mkubwa ambao wamezoea kupitia taarifa za siri katika shughuli zao za kila siku. Hata hivyo, utunzaji wa taaluma binafsi utakuwa ni jukumu la kila mshiriki.
n) LUGHA: Kiswahili kitakuwa ndiyo lugha itakayotumika katika vipengele vyote vya shindano hili, ikiwa ni pamoja na katika kuwasilisha Mpango wa Biashara na uwasilishaji kwa mdomo katika hatua ya fainali. Mafunzo yataendeshwa kwa Kiswahili.

## 4. HATUA/MCHAKATO WA Fankikisha Biashara TEAM Challenge

Fanikisha Biashara TEAM Challenge inaendeshwa katika hatua nne. Maombi yatachambuliwa kuona iwapo yanastahili kushiriki na yamejazwa kwa ukamilifu. Baada ya hapo yatafanyiwa tathmini na timu ya Majaji inayojitegemea.

**<u>Hatua ya 1: Maombi na uchambuzi wa Mipango ya Biashara.</u>**

Waombaji watatuma Fomu za Maombi na Mipango yao ya KUKUZA Biashara kwenda Ofisi ya TECC. Wanaotumia mtandao watafungua na kujaza “online applications” katika mtandao wa TECC:. Maombi ya kupitia barua pepe yatatumwa kupitia anwani za barua pepe zilizoonyeshwa hapo mbele. Mpango wa KUKUZA isizidi kurasa 15 zilizochapwa.

Maombi yote yatapokelewa kuanzia tarehe **19.11.2022 mpaka 02.12.2022**. Mwisho wa kupokea maombi ni Ijumaa, tarehe **02.12. 2022.**
Mpango wa KUKUZA Biashara utafanyiwa uchambuzi na tathmini kutumia vigezo vya wazi ili kupitishwa kuweza kushiriki.

**Hatua ya 2: Mafunzo ya KUKUZA biashara na Utayarishaji Mpango wa Biashara:**

Washiriki watakaopitishwa na kuchaguliwa kushiriki, wataalikwa kushiriki katika semina ya siku tano za mafunzo ya utayarishaji Mpango wa Biashara, ujasiriamali na stadi za maisha. Mafunzo haya yatafanyika katika vituo vya wilaya husika kuanzia tarehe **12.12.2022**. Mafunzo haya yatatoa fursa kwa washiriki kuboresha mipango yao ya Biashara

**Hatua ya 3: Kuunganishwa na walezi wa Kibiashara :**

Kuanzia tarehe **16.12.2022** washiriki wote waliahitimu mafunzo ya siku kumi watapata fursa ya kupata mafunzo ya siku mojaya namna ya kuishi na walezi wa kibiashara na baada ya hapo watapewa mlezi wa kibiashara ili awasaidie katika kuendeleza na kukuza biashara zao hasa katika kutatua changamoto za kila siku . Walezi hawa ni wafanyabiashara wazoefu na wa muda mrefu katika kufanya biashara ,wengine ni wataalamu wa muda mrefu katika kutoa huduma za ushauri katika kukuza na kuendeleza biashara. Washiriki watapata msaada wa kiushauri kutoka kwa walezi wa kibiashara kwa muda wa miezi sita.

**Hatua ya 4 : Kuunganishwa na fursa zingine**

Washiriki watapata nafasi ya kuunganishwa na fursa zingine pale zinapojitokeza za kiujasiriamali hasa taasisi zinazotoa mikopo kwa wajasiriamali kwa masharti nafuu, warsha na makongamano ya kibiashara

## 5. MCHAKATO WA KUCHAGUA WASHINDI

Katika kila hatua uchaguzi wa washindi utafanyika katika kituo kimoja na utafanywa na Timu ya Majaji inayojitegemea. Majaji watachaguliwa kwa uangalifu mkubwa sana.

Uchambuzi utafanyika kwa haki, uwazi na kutumia vigezo vinavyoeleweka.

Majaji watajumuisha Wataalamu waliobobea wa mambo ya biashara, Wajasiriamali waliobobea, Wahadhiri wa Vyuko Vikuu, Weledi wa mambo ya biashara wenye uzoefu wa Uongozi wa Biashara na Mipango ya Biashara. Majaji wote watatakiwa kuhudhuria semina elekezi na wataweka saini Hati ya kuthibitisha kutunza siri.
Mpango wa Biashara Utafanyiwa tathimini na Majaji 2 ili kuondoa uwezekano wa upendeleo. Maamuzi yote kuhusu tathimini yatakuwa ya mwisho, lakini karatasi za kutolea alama zitaweza kupatikana ili kupitiwa na Timu inayojitegemea. Hakutakuwa na nafasi kwa washiriki kukata rufaa.

**6. MITAJI YA FANIKISHA BIASHARA TEAM CHALLENGE.** Washindi watatunukiwa mbegu mtaji kiasi cha fedha zitakazotolewa kama ifuatavyo:

| Idadi ya Waliofunzwa | Idadi ya washindi | Maelezo | Ruzuku kwa kila mshindi (Tsh) | Idadi ya Ruzuku (Tsh) |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | 1 | Mpango bora wa ukuaji wa biashara | Vifaa vya 5M | Vifaa vifaa 5M |
| | 1 | Mpango bora wa ubunifu wa biashara | Vifaa vya 3M | Vifaa vya 3M |
| 36 | 1 | Timu bora ya kike | Vifaa vya 2M | Vifaa vya 6M |
| | 1 | Timu bora kwa ushirikiano | Vifaa vya 1M | Vifaa vya 4M |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 1 | | Vifaa vya 2M | Vifaa vya 4M |
| | | **JUMLA** | **13M** | **13M** |

**7. MAELEKEZO KUHUSU MPANGO WA BIASHARA BIASHARA.**

Tafadhali soma kwa makini kabla ya kuandika Mpango wako wa biashara. Fuata mpangilio wa Fomu ya Maombi. Mpango wa KUKUZA Biashara utaandikwa kwa Kiswahili na itabidi uchapwe kwa Kompyuta kutumia "Times New Roman" ukubwa wa 12 na lisizidi kurasa 15. Mawazo ya biashara yasiyotimiza masharti ya msingi hayatasomwa na yataondolewa kwenye shindano.

9. TAARIFA ZA MAWASILIANO

Ukiwa na swali lolote kuhusu Fanikisha Biashara usisite kuwasiliana nasi kutumia barua

| HALMASHAURI | MHUSIKA | WADHIFA | SIMU | |
|---|---|---|---|---|
| Dodoma- Kondoa | | | | |
| Singida- Iramba | | | | |

MAAFISA WA TECC

1. Godwin Lemunga – Meneja wa Fedha – simu 0712 496689
2. Mwasiti Mkembe – Meneja wa Malezi – simu 0689 874044

**10. HATI YA KUKUBALI KUSHIRIKI KATIKA Fanikisha Biashara (Itumwe TECC)**

Hati ya kukubali kushiriki katika Shindano la Mpango wa Biashara.

Hati hii ya Mkataba wa Ushiriki isomwe na ijazwe ili kuweza Fomu ya Maombi.

Kwa kuomba kwenye kushiriki katika Shindano la Fanikisha Biashara linaloendeshwa na Tanzania Entrepreneurship and Copmetetiveness Centre ninakubali kufuata Masharti yafuatayo:-

**MKATABA WA KUTANGAZWA**

Kwa kujisajili kushiriki katika mashindano, ninakubali kwamba TECC na washiriki wake wana haki ya kuchapisha, kuandika, kutangaza na kutumia ipasavyo katika media yoyote, jina langu, picha yangu, sauti yangu na taarifa yoyote ambayo siyo siri kwa ajili ya kutangaza shughuli za Programu bila malipo yoyote.

**KUKUBALI KUTII SHERIA ZA SHINDANO**

Nimesoma sheria za shindano na kwa kuweka saini yangu katika Hati hii, ninathibitisha kwamba nimekubali na nitatii sheria zote za shindano hili.

**UMILIKI WA MPANGO WA BIASHARA**

Ninakubali na kuthibitisha ya kwamba Wazo la Biashara litakuwa zao la wazo langu binafsi na kwamba sizuiwi na mkataba wowote, wa kisheria au vinginevyo, kutumia Wazo hili la Biashara au kuwasilisha maelezo yake katika shindano.

**KUKUBALI KUFUATA MCHAKATO NA MALENGO YA SHINDANO**

Ninakubali mimi binafsi kutoa muda na rasilimali zangu zingine kuhudhuria mafunzo yote ya shindano la Fanikisha Biashara nitakayoalikwa, kuwasilisha Mpango wa Biashara uliofafanuliwa katika tarehe na muda uliowekwa na Maafisa wanaoendesha shindano kwa ajili ya kufanyiwa tathmini ya kuendelea na shindano. Nikishindwa kufanya hivyo, ninakubali ya kwamba nitapoteza haki zote za ushiriki na nitapoteza Haki zote zinazotolewa kwenye shindano.

**RUZUKU ZA FEDHA**

Zaidi ya hapo ninathibitisha ya kwamba iwapo nitashinda ruzuku ya fedha katika shindano, nitatumia fedha hizo kupanua biashara yangu kulingana na Mpango wa Biashara. Ninafahamu ya kwamba nitaondolewa katika shindano iwapo nitatumia zawadi ya fedha kwenye matumizi yasiyolingana na Mpango wa Biashara. Maafisa wa shindano wanayo haki kupata taarifa juu ya Matumizi ya zawadi.

**KUKANA KUCHUKUA HATUA ZOZOTE ZA KISHERIA**

Ninaelewa na kukubali kwamba Tanzania Cigaratte Company Limited , TECC (Maafisa wa Mashindano), Asasi Shiriki, Wakufunzi, Majaji na Waelekezaji (Wawakilishi wote wa shindano) hawalazimiki kisheria kunipa ushauri au kunipa huduma zozote zisizostahili. Aidha ninathibitisha kwamba maoni na uamuzi utakaofanywa na Majaji ni wa mwisho.

Ninakubali sitawasiliana au kujaribu kuwashawishi Majaji au Wawakilishi wa shindano kufanya uamuzi wa kunipendelea. Ninafahamu ya kwamba jaribio lolote la mawasiliano au kujaribu kushawishi litanifanya nipoteze sifa za kushiriki na hivyo kuondolewa kwenye shindano hili. Vile vile ninakubali kutowahusisha kwa njia yoyote kisheria na ushiriki katika shindano haya. Vile vile ninaelewa na kukubali kwamba Maafisa wa shindano au Wawakilishi wa shindano na TECC hawatahusika na gharama au hasara yoyote ninayoweza kupata kutokana na kushiriki kwangu katika shindano hili.

**KUKUBALI KUTOA TAARIFA ZA BIASHARA**

Kwa Hati hii ya Mkataba wa Ushiriki ninakubali kutoa Taarifa za Biashara ambazo ni muhimu katika ufuatiliaji wa maendeleo ya biashara na ninakubali kushirikiana na wale watakaofanya tathmini ya uendeshaji wa shindano baada ya nusu ya Kipindi na mwisho wa kipindi cha Programu ya Kufanikiwa Kibiashara (TECC).

Ninathibitisha ninaelewa na kukubaliana na masharti ya Hati hii ya Mkataba wa Ushiriki.

Jina Kamili ________________________ Saini ____________________

Mahali __________________ _______ Tarehe ____________________

Iwapo utakuwa na jambo lolote linalohitaji ufafanuzi kuhusu mashindano, usisite kuwasiliana kwa barua pepe, simu au kuonana na wawakilishi wa Makao Makuu ya Programu ya Fanikisha Kibiashara (TECC).